

FAHAMU MAKOSA NA ADHABU ZITOLEWAZO NA SHERIA ZINAZOKATAZA MATUMIZI YA MIFUKO YA PLASTIKI TANZANIA

By Omari Kilwanda-Wakili

Kimsingi kuna **Makosa Makuu Matano** yaliyotajwa na kukatazwa ndani ya Sheria husika. Sheria hiyo Ndogo inajulikana kama **The Environmental Management (Prohibition of Plastic Carrier Bags) Regulations, 2019**. Sheria hii Ndogo imetungwa kwa Mujibu wa **Kifungu Na. 230 (2) (f)** cha Sheria inayojihusisha na Usimamizi wa Mazingira (**The Environmental Management Act, Cap. 191**).

A: MAKOSA

Kwa mujibu wa Kifungu/Kanuni Na. 8 Cha Sheria ya Kuzuia Matumizi ya Mifuko ya Plastiki ambayo ni **The Environmental Management (Prohibition of Plastic Carrier Bags) Regulations, 2019** kuna Makosa Matano ambayo ni;

- (A). Kuzalisha na Kuagiza Mifuko ya Plastiki, **(Kifungu/Kanuni Na. 8 a)**;
- (B). Kusafirisha nje ya nchi Mifuko ya Plastiki, **(Kifungu/Kanuni Na. 8 b)**;
- (C). Kuhifadhi na Kusambaza Mifuko ya Plastiki, **(Kifungu/Kanuni Na. 8 c)**;
- (D). Kuuza Mifuko ya Plastiki, **(Kifungu/Kanuni Na. 8 d)**;
- (E). Kumiliki na Kutumia Mifuko ya Plastiki? **(Kifungu/Kanuni Na. 8 e)**.

B: ADHABU

Kwa kila kosa tajwa hapo juu, Sheria husika imetaja Adhabu yake. Hivyo basi kuna Adhabu aina tano kama ilivyo kwa Makosa husika. Kifungu/Kanuni Na. 8 cha Sheria tajwa hapo juu kilichotaja Makosa Matano ndicho hicho kimetaja Adhabu ya kila Kosa kama ifuatavyo;

(A). Adhabu kwa Wazalishaji na Waagizaji.

Kifungu/Kanuni Na. 8 (a) cha Sheria tajwa hapo juu, kinataja Adhabu kwa Mtu au Watu hao kama ifuatavyo;

- i. Faini isiyopungua **Milioni 20 na isiyozidi Billioni 1**,
- ii. Kifungo Kisichozidi **Miaka Miwili**,

iii. Au vyote **Kifungo na Faini** tajwa hapo juu.

(B). Adhabu kwa Wasafirishaji kwenda nje ya nchi.

Kifungu/Kanuni Na. 8 (b) cha Sheria tajwa hapo juu kinataja Adhabu kwa Mtu au Watu hao kama ifuatavyo;

- i. Faini isiyopungua **Milioni 5 na isiyozidi Milioni 20,**
- ii. Kifungo Kisichozidi **Miaka 2,**
- iii. Au vyote **Kifungo na Faini** tajwa hapo juu.

(C). Adhabu kwa Wanaohifadhi na Wasambazaji

Kifungu/Kanuni Na. 8 (c) cha Sheria tajwa hapo juu kinataja Adhabu kwa Mtu au Watu hao kama ifuatavyo;

- i. Faini isiyopungua **Milioni 5 na isiyozidi Milioni 50,**
- ii. Kifungo Kisichozidi **Miaka 2,**
- iii. Au vyote **Kifungo na Faini** tajwa hapo juu.

(D). Adhabu kwa Wauuzaji

Kifungu/Kanuni Na. 8 (d) cha Sheria tajwa hapo juu kinataja Adhabu kwa Mtu au Watu hao kama ifuatavyo;

- i. Faini isiyopungua **Laki 1 na isiyozidi Laki 5,**
- ii. Kifungo Kisichozidi **Miezi 3,**
- iii. Au vyote **Kifungo na Faini** tajwa hapo juu.

(E). Adhabu kwa Watumiaji na Wanaomiliki

Kifungu/Kanuni Na. 8 (e) cha Sheria tajwa hapo juu kinataja Adhabu kwa Mtu au Watu hao kama ifuatavyo;

- i. Faini isiyopungua **Elfu 30 na isiyozidi Laki 2,**
- ii. Kifungo Kisichozidi **Siku 7,**
- iii. Au vyote **Kifungo na Faini** tajwa hapo.

NB:

SAMBAZA UJUMBE HUU KWENYE MAKUNDI MENGI NA KWA WATU WAKO WOTE ILI KUEPUKANA NA ADHABU ZISIZO ZA LAZIMA. TUSAIDIANE KUTUNZA MAZINGIRA YETU.

Imeandaliwa na **Omari Kilwanda-Wakili,**
KILWANDA C.J & CO. ADVOCATES
0758071970, Kilwanda.adv@gmail.com